HOTUBA YA MHESHIMIWA PROF. IBRAHIM HAMIS JUMA, JAJI MKUU WA TANZANIA KUWAKUBALI NA KUWAPOKEA MAWAKILI - TAREHE 02 DESEMBA, 2022 DAR ES SALAAM

Mheshimiwa Jaji Mustapher Mohamed Siyani, Jaji Kiongozi wa Mahakama Kuu ya Tanzania,

Waheshimiwa Majaji wa Mahakama Kuu,

Mheshimiwa Jaji Dkt. Benhajj Shaaban Masoud, Mkuu wa Taasisi ya Mafunzo ya Uanasheria kwa Vitendo,

Waheshimiwa Majaji Wastaafu,

Prof. Elisante Ole Gabriel, Mtendaji Mkuu wa Mahakama,

Mheshimiwa Wilbert Martin Chuma, Msajili Mkuu wa Mahakama,

Mheshimiwa Sylvester Joseph Kainda, Msajili Mahakama ya Rufani,

Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Elimu ya Sheria,

Bw. Sylvester Anthony Mwakitalu, Mkurugenzi wa Mashtaka,

Dkt. Boniphace Nalija Luhende, Wakili Mkuu wa Serikali,

Mheshimiwa Sharmillah Said Sarwatt, Msajili Mahakama Kuu ya Tanzania,

Bw. Leonard Magacha, Mtendaji wa Mahakama Kuu,

Bw. Michael Marcellus Luena, Rais wa Chama cha Mawakili wa Serikali Tanzania Bara,

Prof. Edward Gamaya Hoseah, Rais wa Chama cha Mawakili wa Tanganyika (TLS),

Waheshimiwa Wasajili, Manaibu Wasajili, Watendaji wa Mahakama na Mahakimu,

Mawakili wa Serikali na Mawakili wa Kujitegemea,
Wanahabari wote,
Wageni Waalikwa,
Mabibi na Mabwana.

Nawasalimu kwa jina la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

Awali ya yote nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, ambaye ameturuzuku Uhai na nafasi ya kukutana pamoja siku ya leo hapa katika viwanja vya Karimjee.

Ni fahari kubwa na heshima kwa Mahakama ya Tanzania kuwakaribisha Mawakili Wapya na familia zenu katika siku ambayo ni muhimu sana katika safari yenu ya elimu na taaluma ya Sheria. Kwa niaba ya Mahakama ya Tanzania, nawapongeza sana na kwa moyo wa dhati, nawakaribisha katika katika wajibu wenu mpya wa uwakili. Siku ya leo inaashiria kukamilika kwa miaka yenu mingi, ya kuitafuta taaluma ya sheria, na kuielewa. Safari hii ndefu iliwahitaji kusoma kwa bidii na kujituma; iliwahitaji kuwa na uvumilivu na pia ustahimilivu. Nawapongeza sana kwa kukubaliwa leo kuwa Mawakili wa Mahakama Kuu na Mahakama za Chini na

kuingizwa rasmi kwenye orodha ya mawakili kuanzia leo tarehe 02 Desemba 2022.

Safari ya Elimu ya Sheria Ni Endelevu na Bado Haijakamilika

Safari iliyobaki mbele yenu ni ndefu na ngumu zaidi kwa kuwa ni safari ya kutumia elimu ya sheria na taaluma ya Uwakili kutatua changamoto mbali mbali za kijamii. Ninasema kuwa safari yenu bado ni ndefu kwa sababu Elimu ya Sheria mliyopata imejengwa kwenye misingi na maudhui ya kutoa huduma za Sheria na Uwakili kwa dunia na Tanzania ya Karne ya 20. Dunia na Tanzania ya leo, ambayo mtatumia elimu na taaluma yenu ya Sheria na Uwakili, ni Dunia na Tanzania katika Karne ya 21. Karne ya 21 haizalishi tena ajira zinazotegemea Elimu yenye maudhui ya Karne ya 20. Karne ya 21 inategemea matumizi makubwa ya teknolojia katika utoaji wa huduma.

Wahitimu waliopata elimu ya sheria yenye maudhui ya karne zilizopita wanahitaji mabadiliko binafsi makubwa, ya kifikra, kimtazamo na ki-mwelekeo. Kwa wale ambao bado hawajui Karne ya 21 inahitaji wahitimu wa aina gani, someni Utangulizi wa Dira ya Maendeleo ya Taifa 2025 na pia someni DIRA yote. Kwa ufupi,

Utangulizi wa Dira ya Maendeleo inatukumbusha kuwa, Karne ya 21 inatawaliwa na wale walio na teknolojia iliyo bora zaidi ya wengine. Yaani ni teknolojia, teknolojia, teknolojia. Inatawaliwa na wanaozalisha mali na huduma zenye tija kubwa zaidi ya wengine. Inatawaliwa na wenye miundombinu ya kisasa na bora ya usafiri na mawasiliano. Inatawaliwa na wenye ujuzi wa hali ya juu, na wenye udhubutu. Kama wewe ni muhitimu wa Karne ya 21, ni lazima uwe tayari kushindana kwa kila kitu na usiwe bingwa wa kulalamika na kulaumu. Lazime utafute namna ya kujiboresha na kujiimarisha maeneo yote ya ushindani. Nawatakia Safari njema katika kutafuta fursa mpya na nyingi katika Tanzania na Dunia ya Karne ya 21.

Hotuba za Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Rais wa TLS

Nawapongeza Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Rais wa Chama cha Mawakili Tanganyika. Viongozi hawa ni wadau muhimu sana wa Mahakama ya Tanzania na katika safari yenu ya Uwakili. Ofisi zao zimetoa mchango mkubwa katika safari yenu ya Elimu ya Sheria hadi kufikia hatua ya kukubaliwa kuwa Mawakili. Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali na ile ya Rais wa Chama cha Mawakili wa Tanganyika itaendelea kuwajenga katika Taaluma na

katika Elimu Endelevu. Hotuba ya Rais wa TLS imetaja juhudi za makusudi zinazofanywa na Baraza la Uongozi chini ya Uongozi wa Profesa Edward Hoseah kushughulikia changamoto za ajira zinazowakabili Mawakili wa Tanzania. Hotuba zilizosheheni nasaha, zilizosomwa na Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Dr. Eliezer Mbuki Feleshi, pamoja na Rais wa Chama cha Mawakili wa Tanganyika (TLS) Prof. Edward Hosea; zitawapa muongozo wa awali kwa sababu Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Rais wa TLS walianza safari ndefu kama nyinyi na nasaha zao zimebeba uzoefu wa muda mrefu sana.

Leo ni siku ya Kuwashukuru Wote waliofanikisha Safari yenu

Ni matumaini yangu kuwa mafanikio yenu yanatokana na juhudi, usaidizi, na msaada kutoka kwa watu mbalimbali wakiwemo wazazi wenu, walezi wenu, ndugu, jamaa, majirani na hata marafiki ambao ni sehemu ya hatua hii mliyofika leo. Hivyo hatuna budi kukumbuka na kuwashukuru wote hao.

Naungana na Mwanasheria Mkuu wa Serikali kuzipongeza taasisi mbalimbali zikiwemo Baraza la Elimu ya Sheria (*The Council for Legal Education*), Vitivo vya Sheria vya Vyuo Vikuu, Shule ya Sheria

Tanzania (*Law School of Tanzania*), Chama cha Mawakili wa Tanganyika, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali, Ofisi na taasisi mbalimbali za umma na binafsi zilizoshiriki katika kuwandaa katika safari yenu ya kufikia daraja la Uwakili leo.

Dhana ya Constructive Engagement

Katika hotuba yake leo hii, na katika hotuba zake tangu achaguliwe kuwa Rais wa TLS, Profesa Edward Hoseah (Rais wa TLS) amekuwa akisisitiza umuhimu wa mashauriano ya kuijenga nchi ya Tanzania ambayo inatumiwa na Baraza la Uongozi la TLS *(constructive engagement).* Hii dhana ya mashauriano *(constructive engagement)* ni njia mojawapo muhimu ya kutekeleza Malengo ya kuanzishwa kwa Chama Cha Wanasheria wa Tanganyika chini ya kifungu cha 4 cha Sheria ya Chama Cha Wanasheria wa Tanganyika *(Tanganyika Law Society Act, Cap. 307).* Malengo ya kuanzishwa Chama Cha Wanasheria wa Tanganyika hayawezi kutekelezwa pale ambapo wahusika hawazungumzi, hawakutani, hawajadiliani, hawashauriani na kuelewana. Kwa lugha ya kiingereza, *"to engage someone to become interested or involved in activity, or to attract someone's interest and keep them thinking."*

Ukosefu wa Ajira kwa wanasheria wanaohitimu elimu ya sheria kwa vitendo ni eneo ambalo linahitaji dhana ya *constructive engagement.* Kila mmoja wenu anafahamu kuwa katika Karne shindani ya 21, Sekta ya Umma (Serikali Kuu, Serikali za Mitaa, Bunge, Mahakama na Mashirika ya Umma) haziajiri idadi ya kutosha ya Mawakili kiasi cha kupunguza Mawakili wasio na ajira. Hata hivyo, Sekta ya Umma ina nafasi na uwezo mkubwa wa kuibua fursa za kibiashara, uwekezaji ambazo zinaweza kuwawezesha Mawakili kushiriki katika Sekta Binafsi hasa katika maeneo mapya ambayo Serikali inayafungua kwa biashara za kitaifa na kimataifa na zile za Uwekezaji Mkubwa ambazo huibua ajira kupitia sekta binafsi. Hapa naona nafasi kubwa ya *constructive engagement.*

MARIANA MAZZUCATO, aliandika kitabu *THE ENTREPRENEURIAL STATE: DEBUNKING PUBLIC VS. PRIVATE SECTOR MYTHS (2015)* ambacho kinasisitiza kuwa Serikali ina wajibu mkubwa wa kuibua na kujenga mazingira stawishi kwa sekta binafsi (na kwa Mawakili na Wanasheria wanaohitimu). Kwa kiasi kikubwa, mazingira stawishi kwa AJIRA KWA MAWAKILI na Wanasheria, inategemea

sana uwekezaji mkubwa utakaofanywa na Dola (Serikali, Bunge na Mahakama).

Hapa Tanzania, kama zilivyo nchi nyingine zinazoendelea, ni Serikali na Sekta ya Umma ndio ina uwezo wa kuweka mazingira stawishi kwa uwekezaji miradi mikubwa ambayo ndio huibua fursa kwa sekta binafsi kujitokeza na sekta binafsi kuibua fursa za ajira. Mfano mzuri hapa Tanzania ni miradi mikubwa inayotekelezwa na SEKTA YA UMMA kwa mfano, miundombinu ya Mawasiliano (Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano, Uwekezaji katika SATELITE za MAWASILIANO) umewezesha makampuni binafsi yanayofanya biashara katika sekta ya mawasiliano kuibuka na kushamiri. Bila uwekezaji katika Mkongo wa Taifa na Internet – Mahakama Mtandao haingekuwepo. Bila uthubutu wa SEKTA YA UMMA katika uwekezaji na katika utafiti katika maeneo ambayo yanahitaji mtaji mkubwa kuwekeza; sekta binafsi hazingejitokeza na kustawi. Kuna faida kubwa kwa maslahi ya ajira ya Mawakili vijana kama Constructive Engagement itatumika kushawishi Serikali iwekeze katika AJIRA MPYA**.** MARIANA MAZZUCATO alitoa mfano wa simu janja *iPhone smartphone* kuwa ni kwa kiasi kikubwa matokeo ya kiasi kikubwa cha fedha zilizotolewa na Serikali ya Marekani

kuwezesha utafiti wa kina *(basic and applied research by the State).* Kwamba, Serikali huingia katika maeneo ya uwekezaji yenye hatari za kupata hasara ambazo sekta binafsi haziwezi kujiingiza.

Mashauriano na majadiliano baina ya Serikali na Chama cha Mawakili wa Tanganyika ni muhimu kutafuta ufumbuzi wa ukosefu wa ajira kwa wanasheria waonaomaliza Elimu ya Sheria kwa Vitendo. Ukosefu wa Ajira ni tatizo kubwa na linahitaji 'engagement' mashauriano, mazungumzo. Jengeni mazingira ya kuaminiwa katika mazungumzo. Dhana ya *constructive engagement* (mazungumzo, majadiliano na mashauriano) baina ya Uongozi wa TLS na Serikali ni muhimu wakati huu ambao Serikali inatayarisha mazingira ya ushiriki wa Tanzania katika Eneo Huru la Biashara la Afrika. Soko hili huria lina fursa kwa Mawakili kupata ajira au kushiriki katika kufanya biashara huru. Hizi fursa ndani ya Eneo Huru la Biashara la Afrika ni zile ambazo Mwanahabari mmoja aitwaye JENNIGAY COETZER alizifikiria alipoandika Makala iitwayo *LAW.COM* aliyoandika tarehe 17/12/2020, aliipa kichwa cha habari- ***"THE AGE OF THE LAWYER: AFRICA'S FREE TRADE DEAL MEANS NEW LAWS, NEW BUSINESS."*** Na akaelezea kuwa:

"Once up and running, the economic bloc of 1.3 billion people will be the world's largest trade zone and is expected to boost Africa's total GDP to over $ 3.4 trillion. It could mean big business for law firms with the right profile."

Mazungumzo, majadiliano na mashauriano ni njia mojawapo ambayo Baraza la Uongozi la TLS inaweza kutumia kuishawishi na kuishauri Serikali, pale inapofanya uwekezaji mkubwa au inapounganisha SOKO la Tanzania kuwa sehemu ya Soko Huru Afrika, ihakikishe kuwa fursa kwa sekta binafsi zinazojitokeza, zinazalisha ajira na zinapunguza uhaba wa ajira kwa Mawakili na Wanasheria wa Tanzania.

TLS Itumie Malengo ya Kuanzishwa kwa kwake Kuishauri Serikali Mbinu za Kuibua Fursa za Ajira kwa Mawakili

Ni jambo lisilo na ubishi kuwa Chama cha Wanasheria Tanganyika TLS ni Chama Huru cha Mawakili ambacho ni chombo chao cha kuendeleza Elimu na Taaluma ya Sheria. Ni ukweli usio na ubishi kuwa Chama Cha Wanasheria wa Tanganyika, kilianzishwa na Sheria MAALUM (*Tanganyika Law Society Act, Cap. 307*) na kupewa

MALENGO YA KISHERIA ambayo yana manufaa makubwa kwa umma. Umuhimu wa TLS kwa maendeleo ya Sheria za nchi yetu Tanzania, ilitambuliwa tangu miaka ya mwanzo ya Uhuru wa Tanganyika. Hii inathibitishwa na maneno, yaliyosemwa na Chief Abdallah Saidi Fundikira (aliyekuwa Waziri wa Sheria, na Mjumbe wa Baraza la Kutunga Sheria akiwakilisha Tabora), wakati wa kusomwa kwa mara ya pili kwa Mswada wa Kurekebisha Sheria iliyoanzisha TLS [*Tanganyika Law Society (Amendment) Bill, 1961*]. Chief Fundikira alisema kuwa TLS sio KLABU binafsi ya Mawakili, kwa manufaa yao binafsi. Alisisitiza kuwa TLS imeanzishwa na Sheria ili kutimiza malengo maalum yaliyowekwa na Sheria.

> *"...We are talking here about the Tanganyika Law Society. It is not that we are talking about a club of advocates for their own perhaps social enjoyment or that sort of thing. But this is a society established by the law of this country and it has to fulfill certain statutory functions."*

Malengo ya kuanzishwa kwa TLS yametajwa kwa ufasaha mkubwa na kifungu cha 4 cha Sheria ya Chama Cha Wanasheria wa Tanganyika *(Tanganyika Law Society Act, Cap. 307)* yanatoa mazingira ya mahusiano baina ya Mahakama, Serikali na Chama Cha Wanasheria Tanganyika kuwa mazuri na yenye manufaa kwa Tanzania. Baadhi ya Malengo ya kuanzishwa kwa TLS ni pamoja na:

> *The objects for which the Society is established are–*
>
> *(a)* **Kuboresha na kulinda viwango vya Taaluma ya Sheria nchini Tanzania** *[to maintain and improve the standards of conduct and learning of the legal profession in Tanzania;*
>
> *(b)* **Kuwasaidia wanasheria na wasio wanasheria kupata maarifa ya sheria** *(to facilitate the acquisition of legal knowledge by members of the legal profession and others);* []
>
> *(c)* **Kuisaidia MAHAKAMA na SERIKALI katika maswala yote yanayohusu Sheria, utawala na uendeshaji na matumizi ya sheria hapa Tanzania** *(to assist the Government and the Courts in all matters affecting legislation, and the administration and practice of the law in Tanzania);*

(d) **Kuwawakilisha, kuwalinda, kuwasaidia na kuwatetea wanasheria kuhusu mazingira ya kufanya kazi zao za kitaaluma** *to represent, protect and assist members of the legal profession in Tanzania as regards conditions of practice and otherwise;*

(e) **Kuwalinda na kuwasaidia wananchi wa Tanzania katika maswala yote yanayohusu au kugusa sheria** *(to protect and assist the public in Tanzania in all matters touching, ancillary or incidental to the law).*

Nawakaribisha Mawakili wapya katika kutekeleza malengo ya kuanzishwa kwa TLS na kutoa huduma muhimu sawa kwa Watanzania. Ukilinganisha aliyoyasema Chief Abdallah Fundikira na malengo ya kuanzishwa kwa TLS yaliyotajwa na Sheria ya TLS utagundua hofu waliyokuwa nayo Wajumbe wa Baraza la Kutunga Sheria ni kwamba TLS isibadilike kuwa KLABU binafsi ya Mawakili yenye malengo na maslahi binafsi nje ya malengo yaliyowekwa na Sheria. Kuna NAHAU ya Kiswahili inayosema, "ANAYEMLIPA MPIGA ZUMARI NDIYE ANAYECHAGUA WIMBO— *He who pays the piper calls the tune.*" Nawasihi Mawakili wapya, tuendelee

kujihadhari na maslahi binafsi yasipindishe malengo ya kuanzishwa kwa TLS.

Miaka 67 imepita tangu sheria iliyoanzisha Chama cha Wanasheria Tanganyika ianze kufanya kazi tarehe 01/01/1955. Hapana shaka, Tanzania ya leo karne ya 21, ni tofauti kabisa na Tanganyika ya nusu ya kwanza ya Karne ya 20 iliyokuwa bado chini ya Utawala wa Waingereza wakati Sheria hii inatungwa. Mazungumzo, majadiliano na mashauriano baina ya Uongozi wa TLS, Vyuo Vikuu, Chuo cha Sheria kwa Vitendo, Baraza la Elimu ya Sheria na Serikali, ndio zinaweza kuzaa maboresho ya Sheria ya Mawakili *(Advocates Act, Cap. 341)* na Sheria ya Chama cha Mawakili Tanganyika ili zilingane, sio tu na matarajio ya Mawakili wa Karne ya 21 bali pia maslahi ya wananchi wa Tanzania wa karne ya 21.

UWAKILI NI MAADILI, UWEZO, UMAHIRI NA HUDUMA BORA

Ukisoma Kanuni zenu za Maadili ya Kitaaluma [*Advocates (Professional Conduct and Etiquette) Regulations, 2018 GN 118/2018*], utagundua kuwa uwakili ni uadilifu *(integrity)*. Uwakili ni umahiri na huduma bora *(competence and quality of service)*. Uwakili ni uaminifu na unyoofu *(honesty and candour)*, na Uwakili

unahitaji **usiri** *(confidentiality).* Kila Wakili ni lazima awe na vigezo hivyo vyote kwa pamoja. Unaweza kupoteza sifa ya uwakili ukionekana huna UADILIFU, huna UMAHIRI, wewe sio mwaminifu, sio mnyoofu, mropokaji wa siri za wateja.

Nawashukuru sana, Mwanasheria Mkuu wa Serikali Mhe Dkt. Eliezer Mbuki Feleshi, na Rais wa TLS (Profesa Edward Hoseah) kwa kuwakumbusha Mawakili wapya na wale wa zamani kuhusu umuhimu wa Kanuni za Maadili zinazoongoza kazi ya mawakili. Kila anayekubaliwa kuwa WAKILI, anachukuliwa kuwa amejifunga na SHERIA na KANUNI zote zinazoongoza maadili. Swala la UADILIFU *(Integrity)* limepewa umuhimu na uzito wa kipekee na Kanuni za Maadili ya Mawakili wa Kujitegemea. Kanuni ya 4 ya Kanuni za Maadili ya Mawakili wa Kujitegemea inamtaka KILA WAKILI awe ni mtu MUADILIFU. Kanuni ya 6, imeainisha jumla ya mambo 17, ambayo WAKILI akiyafanya anachukuliwa moja kwa moja kuwa amepoteza SIFA YA UADILIFU na pia UWAKILI wake. Kanuni ndogo ya **6(o)**, inawataka Mawakili kupima kila neno wanalotamka au kuandika. Kanuni hii inakataza Mawakili kutamka jambo bila kujali kama ni kweli au sio kweli. Kanuni hii inawakataza kutoa matamshi ya dharau dhidi afisa wa mahakama;

dhidi ya wakili mwenzako, au kiongozi wa umma au dhidi ya wananchi. Mawakili wenye hulka ya kudakia kila ajenda inayojitokeza kabla ya kuilewa, huingia ndani ya mtego wa kanuni hii.—

> *6"(o) knowingly, or with reckless disregard for the truth, makes any false or disparaging or misleading statement against any judicial officer, fellow advocates, public leaders or any other member of the public;"*

PELEKENI HUDUMA ZA MAWAKILI MAENEO YOTE YA TANZANIA

Mahakama ya Tanzania inaendelea na juhudi thabit za kusogeza huduma ya utoaji haki karibu na wananchi. Tangu mwaka 2015 Mahakama ya Tanzania imejenga majengo ya kisasa kutoa huduma za Mahakama katika mikoa yote ya Tanzania. Hivi karibuni nilizindua majengo ya Mahakama za Wilaya katika wilaya zipatazo ISHIRINI (20) kama ifuatavyo; (1) MWANGA (Mkoa wa Kilimanjaro), (2) SAME (Mkoa wa Kilimanjaro), (3) BUSEGA (Mkoa wa Simiyu) (4) ITILIMA (Mkoa wa Simiyu), (5) BUTIAMA (Mkoa wa Mara), (6) RORYA (Mkoa wa Mara), (7) SONGWE (Mkoa wa Songwe), (8) GAIRO (Mkoa wa Morogoro), (9) MKINGA (Mkoa wa Tanga), (10) MBOGWE

(Mkoa wa Geita), (11) NYANG'HWALE (Mkoa wa Geita), (12) KYERWA (Mkoa wa Kagera), (13) MISSENYI (Mkoa wa Kagera), (14) KALIUA (Mkoa wa Tabora), (15) UVINZA (Mkoa wa Kigoma), (16) BUHIGWE (Mkoa wa Kigoma), (17) KAKONKO (Mkoa wa Kigoma), (18) TANGANYIKA (Mkoa wa Katavi), (19) KILOMBERO (Mkoa wa Morogoro), na (20) MVOMERO (Mkoa wa Morogoro). Kati ya Mahakama hizo Mahakama KUMI NA NNE (14) ni Mahakama mpya ambazo zinaanza kutoa huduma ya ki-Mahakama kwa mara ya kwanza. Mahakama hizo ni; (1) BUSEGA, (2) ITILIMA, (3) BUTIAMA, (4) RORYA, (5) SONGWE, (6) GAIRO, (7) MKINGA, (8) MBOGWE, (9) KYERWA, (10) MISSENYI, (11) KALIUA, (12) UVINZA, (13) BUHIGWE, na (14) KAKONKO.

Kuzinduliwa kwa majengo ya Mahakama hizo pamoja na nyingine zitakazozinduliwa kabla ya mwisho wa mwaka huu (2022) ni fursa tosha kwenu mawakili wapya kwenda katika wilaya hizi na kusogeza huduma zenu muhimu za uwakili karibu na zaidi na wananchi.

Aidha, kwa kuwa baadhi ya wilaya hizo ni mpya bado zipo fursa nyingi nyingine za kiuchumi ambazo mnaweza kuzitumia ili kujipatia kipato. Hivyo nawashauri hameni kutoka mijini na katika majiji ambako soko la uwakili lina ushindani mkubwa hasa kwa mawakili ambao bado hawajapata uzoefu wa kutosha.

HITIMISHO

NAWAKARIBISHA MAWAKILI WAPYA KATIKA KAZI MUHIMU YA UWAKILI

MUNGU AWABARIKI, ASANTENI KWA KUNISIKILIZA